# LEARNING BY EAR.

## Lent Luxury-The risks of raising credit.

## EPISODE SEVEN: THE LEGAL RISK.

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**LIST OF CHARACTERS BY SCENE:**

**SCENE ONE:GORI ARRESTED IN KWANZA PUB.**

- **NARRATOR(M 30)**
- **3-5 BAR CUSTOMERS (M, > 20)**
- **GORI(M 45)**
- **BAR MAN(M 30’S)**
- **CUSTOMER(M 30’S)**
- **OFFICER(M 50)**
- **JENNY(F 15)**
- **JD(M 15)**

**SCENE TWO: COURTROOM,UNCLE BARRY IMPRISONED.**

- **UNCLE BARRY(M 45)**
- **JUDGE ALICE( F 40’S)**
- **PROSECUTOR(M 40’S)**
- **4-5 PEOPLE IN AUDIENCE (M/F ALL AGES) / “CROWD”**
- **NARRATOR (M 30)**

**SCENE THREE: AT THE POLICE STATION.**

- **JENNY (F 15)**
- **JD( M15)**
- **GIDDY(M 15)**
- **OFFICER(ADULT M/F)**

**SCENE FOUR: OFFICE IN POLICE STATION.**

- **OFFICER (M 50)**
- **SECRETARY(F 20’S)**

**SCENE FIVE:AT JD’S.**

- **NARRATOR(M 30)**
- **NINA(F 35)**
- **LUKA(M 35)**

**INTRO:**

**1. SFX: OFFICE AMBIENCE.**

**2. NARRATOR:**

Hujambo na karibu katika mfululizo wa vipindi hivi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako. Mimi ndiye mhusika mkuu katika mchezo huu wa Redio ‘Starehe za Kuazima- Tatizo la kugharamia Mkopo’ Na jina Langu.......

**3. SFX: PHONE RINGS**

**4. NARRATOR:** Sahamani, dakika moja tu....

**5. SFX: PHONE PICKED UP**

**6. NARRATOR:**

Gideon Leboo, ofisa anayehusimamia masuala ya mikopo katika benki hii. Nikusaidie na nini? Subiri kidogo nikuunganishe.

**7. SFX: PHONE DIALED AND HUNG UP**

**8. NARRATOR:**

Samahani, tusahau mambo ya simu sasa na tugeukie hadithi kuhusu maisha yangu ya ujana na jinsi nilivyojikuta mashakani. Katika kipindi

kilichotangulia, nilikueleza jinsi wazazi wangu walivyokuja kujua nimeiba Redio ya Mjomba Barry na kuiweka kama dhamana ili tuweze kupata mkopo wa kulipa deni la rafiki yangu JD. Baadaye, Familia yangu inavamiwa na majambazi wawili waliokuwa wakimtafutaMjomba Barry ambaye tumekuja kufahamu kwamba yuko mashakani zaidi. Maafisa wa usalama wanafanikiwa kuwatia mbaroni majambazi hao .Pia wanatuahidi kumsaka Gori ambaye alimvunja Mkono rafiki yangu Jenny akidai deni lake. Hatimaye walifanikiwa kumkamata mlaghai huyu akiwa amejificha katika mgahawa mmoja kijijini -Kwanza …

**SCENE ONE:GORI ARRESTED IN KWANZA PUB**

**9. ATMO: LOCAL PUB AMBIENCE**

***KW begin***

**10. GORI: (Drunk)** Wewe mhudumu, nipe pombe.

**11. BAR MAN:(Confused)** Subiri kidogo!

**(To another customer)** Umenipa pesa ngapi?

**12. CUSTOMER: (Chuckles)** Dola mbili. Na hata pesa bado uko nazo mkononi.

**13. BAR MAN:(Realises)** Uh! Nimechanganyikiwa mjinga mimi! Sijui kwanini nimechanganyikiwa hivi leo!

***KW end***

14. **GORI:** **(Rudely)** Niletee pombe! Una shida gani, kwani pesa zangu hazina thamani au vipi?

15. **BAR MAN:** Subiri dakika moja tu, sawa? Wateja ni wengi sana wanasubiri kuhudumiwa sio wewe peke yako!

16. **SFX:** **HEAVY FOOTSTEPS ENTER. THE PATRONS GO SILENT**

17. **OFFICER:** Ni ...yule.?

18. **JENNY:** Ndio, ni yule..

19. **JD:** Yule ni Gori.

20. **OFFICER:** Gori, kuanzia sasa uko mikononi mwa maofisa wa usalama kwa kosa la kuwalaghai vijana hawa na kumvunja mkono Jenny. Na usijaribu kutoroka maana hutafika mahali popote.

21. **GORI:** **(Drunkenly)** Hakuna mtu anayeweza kumtia mbaroni Gori!. Usijaribu kunitisha!

22. **SFX:** **HANDCUFFS JINGLE.**

23. **OFFICER:** Nyosha mikono yako !

24. **GORI:** Hebu niache.! Niache! Mimi si mwizi!

25. **OFFICER:** Twende!

26. **SFX:** **COMMOTION AS HE IS DRAGGED AWAY**

27. **BAR COSTUMERS: (Murmur as the chief and his quarry leave)**

## 28. NARRATION

Lakini huo ndio uliokuwa mwanzo tu wa sheria kuchukua mkondo wake. Siku mbili baadaye Mjomba Baary akakamatwa katika kijiji kimoja sio mbali sana na mahali tulipokuwa tukiishi. Rafiki wa zamani wa Mjomba Barry, Bw. Mando alikuwa ametoa ripoti kwa maofisa wa polisi kuhusu kisha cha kutapeliwa na mjomba. Kama ningekuwa ofisa wa masuala ya mikopo wakati huo, ningemshauri mjomba Barry ajaribu kubana matumizi na kuongeza kiwango cha akiba. Wakati mtu anapokabiliwa na hali ngumu ya kifedha, jambo muhimu ni kupunguza matumizi na kutafakari hali yake ya kifedha. Ni bora uchukue kalamu na ili kupanga matumizi yake: upande mmoja kiasi cha pato lake la kila mwezi na upande mwengine matumizi na njia bora za kubana matumizi hayo. Ikiwezekana aongeze kama akiba, katika hali hii mtu ataweza kuongeza pato lako! Isitoshe pia unahitajika kutafuta njia nyingine ya kuongeza kipato chako. Ni bora zaidi kuliko kukimbia huku na huko ukitafuta mikopo na hatimaye kuishia kama mjomba Barry.

**SCENE TWO: COURTROOM, UNCLE BARRY IMPRISONED.**

29. **ATMO: COURTROOM AMBIENCE, MURMURS.**

30. **SFX: GAVEL HITS HARD SURFACE.**

31. **JUDGE ALICE:** Kimya kotini!

32. **SILENCE.**

33. **JUDGE ALICE:** Kiongozi wa Mashtaka.

34. **PROSECUTOR:** Ndio mheshimiwa!

35. **JUDGE ALICE:** Unaweza kuendelea na kesi.

36. **PROSECUTOR:** Mheshimiwa,imekuwa tabia ya baadhi ya watu kuchukua mikopo na kisha kutoweka bila kulipa pesa hizo. Watu wengine kama mshtakiwa hapa hufikia kiwango cha kuwa tapeli, kulaghai benki au hata kuwaibia wengine kutokana na ulevi wa kupindukia, na kucheza kamari, jambo linaloweza kuepukika! Hivyo naiomba mahakama hii kumpa adhabu kali mshtakiwa ili iwe funzo kwa wengine wenye tabia ya aina hii. Ni hayo tu mheshimiwa!

37. **CROWD: MURMURS.**

38. **SFX: GAVEL HITS TABLE.**

39. **JUDGE ALICE:** Kimya! ..Barnabas Leboo, una chochote cha kuongezea?

40. **UNCLE BARRY:** **(meekly)** Mheshimiwa nadhani nimesema yote niliyokusudia kusema mahakamani.

41. **JUDGE ALICE:** Katika kesi hii nambari 595/7, Barnabas Leboo unashtakiwa kwa kujipatia kiasi cha dola 400 kutoka kwa Bw. George Mando kwa njia ya udanganyifu, na kulaghai benki, ukiwa na nia ya kutoweka na pesa hizo. Hivyo mahakama hii imekupata na hatia na kukuhukumu kifungo cha miaka miwili gerezani! Pia ukiwa gerezani, utalazimika kuhudhuria vikao vya kila wiki ili kujifunza mbinu za kujirekebisha tabia yako ya ulevi wa kupindukia maisha ya kucheza kamari na kuchukua mikopo usiyoweza kulipa. Maofisa wa mahakama mhakikishe maagizo haya yanafuatwa kikamilifu. Koti imekamilisha kutoa uamuzi wake!

42. **UNCLE BARRY:** Oh hapana, haiwezekani! Mimi si mhalifu, hapaaaaana! Hapaana!

43. **SFX:** **RUSTLE OF CLOTHES AND FEET AS PEOPLE STAND UP.**

44. **NARRATOR:**

Kwa hivyo Gori, wale majambazi wawili na mjombangu Barry wakakabliwa na mkono wa sheria kutokana na

vitendo viovu. Lakini kwa upande wetu, kama tulifikiri tumeepuka mkono huo wa sheria,basi tulikuwa tunakosea. Kwani maofisa wa polisi walituhukumu adhabu ya kukata nyasi na kusafisha kituo hicho cha polisi kwa muda wa wiki moja. Mjomba Barry, pia alipaswa kuhudhuria vikao hivyo vya kurekebisa tabia dhidi ya kuchukua mikopo bila mipangilio!

**SCENE THREE: AT THE POLICE STATION**

**45. SFX: GRASS BEING CUT BY MACHETES.**

**46. JENNY:** **(Complaining)** Yote haya ni kwasababu ya kuchukua mikopo bila mpangilio!.

**47. JD:** Unalalamika nini? Kazi yako wewe itakuwa ni kuokota makaratasi na sisi kukata nyasi kwa muda wa wiki nzima!

**48. JENNY:** **(Not amused)** Ni kweli! Lakini wewe ndio chanzo cha mimi kuvunjika mkono. Yote haya ni kwasababu ya wewe!

**49. JD:** Sikiliza Jenny, mimi sikuwepo wakati ukivunjika mkono!

**50. JENNY**: Lakini wewe ndio chanzo ya haya yote! Kama hungetumia njia za udanganyifu kuigiza sahihi ya

babako ili uweze kuchukua baiskeli kwa mkopo, haya yote hayangetokea!

**51. GIDDY:** Kulitokea nini,...? kulitokea nini? Badala ya kulaumiana, tunapasaa kujipa moyo na kushauriana!

**52. JENNY:** Kuhusu nini?

**53. GIDDY:** Kuhusu njia bora za kuishi bila kuchukua mikopo

**54. JD:** Na ni vipi tunaweza kuepukana na mikopo hiyo?

***KW begin***

**55. GIDDY:** Njia mojawapo ni kujiepusha na maisha ya hali ya juu zaidi ya uwezo wetu.

**56. JENNY:** Kumaanisha?

**57. GIDDY:** Kumaanisha hatuwezi kuishi maisha tusiyoweza kumudu, eti kwa sababu tunataka kuiga maisha ya wengine!

**58. JD:** Nimekuelewa.

***KW end***

**59. GIDDY:** Mfano mzuri, JD, alikuwa hana lazima ya kwenda kuchukua baiskeli kwa mkopo eti kwa sababu unataka kuonekana ukiishi maisha ya juu kama wengine shuleni!

**60. JD:** Kwa hiyo unasema ningeendelea kutembea kwenda shuleni maisha yangu yote?

**61. GIDDY:** Ukiwa huwezi kununua basi sahau kabisa mambo ya kuchukua mkopo! Kuna haja gani ya kununua kitu kwa mkopo na kisha kuishia hali tuliyo sasa? Jenny amevunjika mkono! Na sisi tumeishia kufanya kazi katika kituo cha polisi kama wahalifu.

**62. OFFICER: (Calls from far)** Nyinyi watoto, fanyeni kazi, au mnataka nije hapo sasa hivi!

**63. SFX: MACHETES CUTTING GRASS AS THEY GET BACK TO WORK.**

**<u>SCENE FOUR: AT THE POLICE STATION</u>**

**64. ATMO: POLICE STATION, INSIDE**

**65. SFX: OLD-FASHIONED OFFICE TELEPHONE RINGS.**

**66. SECRETARY:** Hallo? Hapa ni kituo cha polisi... sawa subiri kidogo. **(To the officer)** Ni simu yako.

**67. OFFICER:** Ni nani?

**68. SECRETARY:** Anasema anaitwa Mando, anajibu simu yako…

**69. OFFICER:** Hallo Bw Mando..Naam,....Mmh. ndio, naam sababu kubwa ya kukupigia simu , nilitaka ufike hapa kituoni ili

kuwapa mafunzo wanafunzi wa Shule ya- Kwanza, kuhusu njia bora za kujiepusha na hatari ya kuchukua mikopo au kujilimbikizia madeni! Naam najua utatumia ujuzi wako wote kuwasaidia hawa vijana wa kijiji ! Kumekuwa na visa vingi vya watu kuchukua mikopo isiyo na mipango, au kujilimbikizia madeni wasiyoweza kuyalipa! Hapa tayari nina kesi nyingi sana kuhusu visa vya aina hii. Nitashukuru sana…. **(pause).** Asante na kwaheri.

**SCENE FIVE: AT JD'S.**

**70. NARRATOR:**

Jioni hiyo, babake JD, Bw. Luka anafika nyumbani baada ya kuwa safarini kumtembelea kakake anayeugua. Na kabla ya kufika nyumbani, tayari anafahamishwa yote yaliyotokea kijijini mwao cha Kwanza. Hebu fikiria alivyochemka kwa hasira.

**71. SFX: VILLAGE AMBIENCE, CATTLE MOOING, SOMEONE MILKING.**

***KW begin***

**72. NINA:** **(Talks to the cow)** Njoo hapa Maridadi! Njoo hapa, nataka kumaliza kazi hii ya kukukamua kabla ya kufanya kazi nyingine.

**73. SFX: MARIDADI THE COW MOOS.**

**74. NINA:** Ng’ombe mzuri! Sawa!

***KW end***

**75. SFX: COW BEING MILKED, FOOTSTEPS APPROACH**

**76. LUKA:** **(Speaks suddenly and startles Nina)** Nasikia sasa mtoto wako ni jambazi anayetafutwa?

**77. NINA:** **(Startled)** Luka! Umenishtua! Usininyapie jinsi hiyo!

**78. LUKA**: **(Not amused)** Nimekuuliza swali!

**79. NINA**: Luka! Yaani huwezi kunisalimia hata baada ya kuwa safarini kwa muda wote huo wa wiki mbili? Unaongea na mimi kana kwamba tumekuwa wote tangu asubuhi.

**80. LUKA**: Yuko wapi? Yuko wapi JD?

**81. NINA**: Yuko ndani chumbani!  Amerudi sasa hivi kutoka kituo cha polisi..

**82. LUKA**: **(With finality)** Mwambie sitaki kumuona hapa nyumbani kwangu!

**83. SFX: FOOTSTEPS AS LUKA LEAVES**

**84. NINA:** Luka! Subiri kidogo! JD ni mtoto wako! Huwezi kumfukuza mtoto wako jinsi hiyo!

**85. LUKA:** **(from far)** Kama unataka aishi hapa, lazima alipe redio nayoambiwa aliiba.

**86. NINA:** Lakini si yeye peke yake! Walikuwa pamoja na Gidyy na Jenny! Hawezi kuilipa peke yake!

**87. LUKA:** Lakini naambiwa yeye ndiye chanzo cha yote hayo. Sivyo?

**88. NINA:** Luka, huwezi kufanya hivyo!

**89. LUKA:** Naweza na nitafanya! Wacha kwanza nifike kwenye karakana yangu kuangalia jinsi wafanyi kazi wangu wanavyoendelea na kazi. Lakini nitakaporudi sitaki kumuona hapa!

**90. SFX: FOOTSTEPS LEAVING**

**91. NINA:** Luka… Luka?

**<u>OUTRO</u>:**

**92. SFX: OFFICE AMBIENCE.**

**93. NARRATOR:**

Na hapo Babake JD akaondoka bila ya kuangalia Nyuma! Nina akiachwa amesimama na kibuyu chake cha maziwa. Sasa JD atapata wapi pesa za kulipa madeni yake? Ataishi wapi baada ya babake kutisha kumfukuza nyumbani? Hayo ndiyo nitakayokuwa nikimsimulia wakati nitakaporejea katika kipindi kinachofuata. Ukiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu: dw.de/lbe. Asante kwa kutusikiliza, hadi wakati mwengine, Kwaheri kwasasa!